

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

.....
HALMASHAURI YA WILAYA YA NGARA
(Barua zote ziandikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)

Simu: 028 2226016,
Nukushi: 028 2226152,
Barua pepe: ded.ngara@kagera.go.tz
ded@ngaradc.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
S.L. P. 30,
NGARA

Kumb.Na.NGR/DC/CD/GNR/06/151

15/11/2018

AFISA MTENDAJI KATA,

KATA YA _____
NGARA.

**YAH: VIKUNDI VYA KIJAMII, UCHUMI NA SANAA VILIVYOKO KATIKA KATA NA
VIJJI VILIVYOKO NDANI YA KATA YAKO.**

Tafadhali husika na somo tajwa hapo juu.

Zoezi la kupitishia vikundi vya kijamii, uchumi na sanaa vilivyoko katika kata na vijiji vilivyoko ndani ya kata yako ili viweze kusajiliwa na kupitisha maombi ya mikopo ili kuweza kuendelea na utaratibu unaofuata katika ngazi ya wilaya katika idara ya Maendeleo ya Jamii, limekuwa likifanyika kwa kasi nzuri, lakini zoezi hili limeweza kuleta changamoto mbalimbali ambazo zinatokana na kutokuwepo kwa uhalisia wa vikundi hivyo na shughuli wanazozifanya.

Changamoto zinazojitokeza ni zifuatazo:-


1. Vikundi vingi mnavyovipitishia kusajiliwa na kupatiwa mikopo havina sifa zinazostahili hawana shughuli za pamoja kama kikundi.
2. Umri wa wanavikundi hasa vya vijana wengi wao ni zaidi ya miaka 35, na umri unaotakiwa ni kuanzia miaka 15 hadi 35. Zaidi ya hapo hao ni wazee.
3. Vingi ni vikundi hewa vikitembelewa mahali vilipo wanavikundi hawapatikani, hivyo wakipewa mikopo hugawana na kuhamia nje ya ngara na kushindwa kurejesha mikopo waliyopewa, hasa kwa vikundi vya vijana.
4. Wengine huchukuana wanafamilia na kuomba kusajiliwa kama kikundi.
5. Idadi ya wanakikundi ni kuanzia watu 5 hadi 30, wengi wao huwa chini ya 5 na mikopo unapotolewa hunufaisha mtu mmoja au wawili na inapofikia muda wa kurejesha sababu mbalimbali hutolewa kwamba wengine walichukua fedha na kuondoka, wengine walifariki nk.

Changamoto hizi zimesababisha vikundi hivi kushindwa kurejesha mikopo waliyopewa na dhana ya mzunguko wa fedha za mikopo kwa vikundi kushindwa kutekelezeka yaani **"Revolving fund"**, na wakati mwingine kusababisha vikundi kupelekwa mahakamani ambapo ni kinyume cha taratibu na kanuni za mikopo ya vijana, wanawake na walemavu.

Kwa kuwa wewe unafanya kazi katika kata na kusimamia vijiji vyote vilivyoko ndani ya kata yako kwa usimamizi wa Maafisa watendaji wa vijiji (VEO) kwa niaba ya Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya wilaya, unatakiwa kuwa makini na kujiridhisha kwa kufika katika kikundi hicho na kujionea shughuli za kiuchumi wanazozifanya na kutathmini kama wakipewa mikopo walioomba wataweza kurejesha kwa kutumia shughuli zao za uzalishaji mali. Ikiwezekana fanya hata utafiti/ upelelezi wa kikundi husika kwa jamii ya wananchi wa eneo hilo ili kuweza kupata taarifa zao zilizo sahihi ndipo utaratibu wa kuwapitishia au kutowapitishia uendele. Kwa vikundi utakavyobaini kuwa havina sifa na kusitisha utaratibu wa kutoendelea wapewe sababu na maeneo ya kufanyia kazi ili nao waweze kutimiza masharti na hatimae kupata haki ya kusajiliwa na kupatiwa mikopo ili kuweza kujikwamua kiuchumi. Kushindwa kufanya hivyo na kusababisha kuwepo kwa vikundi hewa wakati umewapitishia na maafisa watendaji wa vijiji, basi wewe ndiye utakayewajibishwa.

Katika mikutano na vikao kwa ngazi zote za kata, vijiji na vitongoji uhamasishaji wa wananchi kuunda vikundi iwe ni agenda ya kudumu, pia kuna maeneo hayana kabisa vikundi hasa katika kata za Keza, Nyamagoma, Muganza na Kibogora, kata hizi zinahitaji uhamasishaji wa hali ya juu ili nao wanaufaike na fedha hizi za mikopo, kwani serikali itasaidia wananchi wake kujikwamua kiuchumi wakiwa kwenye vikundi na si mtu mmoja mmoja. Na kuanzia **tarehe 01/07/2018 vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu vitakopeshwa bila ya Riba**, hivyo kiasi kitakachokuwa kikitolewa ndicho hichohicho kitakachorejeshwa kwa muda wa mwaka mmoja. **Hii ni Sheria ya Fedha No. 4 ya mwaka 2018 ambayo imeifanyia marekebisho Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (The Local Government Finance ACT).**

Nikutakie utekelezaji mwema katika kuhakikisha vikundi halisi na vyenye sifa ndivyo vinavyonufaika na fedha za mikopo ya asilimia 10% inayotokana na makusanyo ya ndani ya halmashauri kwa maendeleo ya wananchi wa Ngara.


Aidan J. Bahama,
MKURUGENZI MTENDAJI (W),
MK **NGARA** MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
NGARA

Nakala: Mh. Diwani,
Kata ya _____
NGARA.

SIFA ZA VIKUNDI.

1. VIKUNDI VYA WANAWAKE:

- i. Kikundi kiwe cha watu 5 – 30.
- ii. Kikundi kiwe cha wanawake tu kuanzia miaka 18 na kuendelea (Lakini hata kama kuna binti mwenye mtoto kabla ya kufikisha miaka 18 anaruhusiwa kujiunga katika kikundi kwasababu tayari ana sifa ya mwanamke).
- iii. Kikundi kiwe na mradi/ miradi endelevu itakayowezesha kurejesha mkopo.
- iv. Kikundi kiwe kimesajiliwa rasmi na kupewa namba ya usajili na halmashauri kupitia idara ya maendeleo ya jamii.
- v. Wanakikundi wawe wanaishi katika mazingira ya karibu ili katika shughuli za pamoja za kikundi na kukutana kwaajili ya mikutano na vikao iwe rahisi kwa kila mmoja kshiriki.
- vi. Kikundi kiwe na Akaunti Benki ili wanapopata mkopo wawekewe fedha zao benki.
- vii. Kikundi kinatakiwa kutuma maombi ya mkopo kwa Mkurugenzi mtendaji wa wilaya na kupitishwa na Afisa mtendaji wa kata na kijiji mahali kikundi kilipo. (Watumishi hawa ndio wanaotakiwa kuvikagua vikundi ka niaba ya mkurugenzi ili kujiridhisha na sifa kabla ya kupitisha maombi yao).
- viii. Wanakikundi wote wawe raia wa Tanzania.
- ix. Kikundi kisiwe cha wanafamilia.

2. VIKUNDI VYA VIJANA:

- i. Kikundi kiwe cha watu 5 – 30.
- ii. Kikundi kiwe cha vijana wa kike na wa kiume umri kuanzia miaka 15 – 35.
- iii. Kikundi kiwe na mradi/ miradi endelevu itakayowezesha kurejesha mkopo.
- iv. Kikundi kiwe kimesajiliwa rasmi na kupewa namba ya usajili na halmashauri kupitia idara ya maendeleo ya jamii.
- v. Wanakikundi wawe wanaishi katika mazingira ya karibu ili katika shughuli za pamoja za kikundi na kukutana kwaajili ya mikutano na vikao iwe rahisi kwa kila mmoja kshiriki.
- vi. Kikundi kiwe na Akaunti Benki ili wanapopata mkopo wawekewe fedha zao benki.
- vii. Kikundi kinatakiwa kutuma maombi ya mkopo kwa Mkurugenzi mtendaji wa wilaya na kupitishwa na Afisa mtendaji wa kata na kijiji mahali kikundi kilipo. (Watumishi hawa ndio wanaotakiwa kuvikagua vikundi ka niaba ya mkurugenzi ili kujiridhisha na sifa kabla ya kupitisha maombi yao).
- viii. Wanakikundi wote wawe raia wa Tanzania.
- ix. Kikundi kisiwe cha wanafamilia.

3. VIKUNDI VYA WATU WENYE ULEMAVU:

- i. Kikundi kiwe cha watu 5 – 30.
- ii. Kikundi kiwe cha watu wenye ulemavu wa viungo, ngozi, masikio, macho na mtindio wa ubongo kwa umoja wao wa Shirikisho la Vyama vya watu wenye ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA).
- iii. Kikundi kiwe na mradi/ miradi endelevu itakayowezesha kurejesha mkopo.
- iv. Kikundi kiwe kimesajiliwa rasmi na kupewa namba ya usajili na halmashauri kupitia idara ya maendeleo ya jamii.
- v. Wanakikundi wawe wanaishi katika mazingira ya karibu ili katika shughuli za pamoja za kikundi na kukutana kwaajili ya mikutano na vikao iwe rahisi kwa kila mmoja kshiriki.
- vi. Kikundi kiwe na Akaunti Benki ili wanapopata mkopo wawekewe fedha zao benki.

- vii. Kikundi kinatakiwa kutuma maombi ya mkopo kwa Mkurugenzi mtendaji wa wilaya na kupitishwa na Afisa mtendaji wa kata na kijiji mahali kikundi kilipo. (Watumishi hawa ndio wanaotakiwa kuvikagua vikundi ka niaba ya mkurugenzi ili kujiridhisha na sifa kabla ya kupitisha maombi yao).
- viii. Wanakikundi wote wawe raia wa Tanzania.
- ix. Kikundi kisiwe cha wanafamilia.